(18)

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA

Barua pepe: rbclindi@pccb.go.tz
Wavuti : www.pccb.go.tz
Simu ya Bure : 113

TAKUKURU Mkoa,
S. L. P 1004,
Lindi.

TAARIFA KWA UMMA

MALIPO PUNGUFU YA POSHO ZA KUJIKIMU KWA WALIMU WA AJIRA MPYA YAOKOLEWA

Lindi
Julai , 2024

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2024 TAKUKURU Mkoani Lindi ilifanikiwa kuokoa fedha kiasi cha Shs. 8,541,500.00 kutokana na uchunguzi uliofanyika kuhusiana na malipo ya posho ya kujikimu ya walimu wa ajira mpya halmashauri ya Mtama.

Fedha hiyo iliyookolewa inatokana na mapunjo ya malipo yaliyofanyika kwa walimu ishirini na saba (27) wa ajira mpya ya Julai, 2022 kupitia akaunti za walimu hao. Afisa elimu Sekondari na Mhasibu wa Halmashauri ya Mtama walifanya malipo hayo baada ya TAKUKURU Lindi kuanzisha uchunguzi kuhusiana na mapunjo ya malipo ya fedha za kujikimu yaliyostahili kufanyika kwa watumishi hao wa ajira mpya kada ya ualimu idara ya elimu Msingi na Sekondari katika halmashauri ya wilaya ya Mtama.

Halmashauri ya Wilaya ya Mtama ilipokea fedha ya kuwezesha watumishi hao posho ya kujikimu ya siku saba (7) na nauli ya usafiri kwenda kuanza kazi katika vituo walivyopangiwa. Halmashauri hiyo ilifanya malipo pungufu kwa watumishi hao ya Jumla ya Shs. 17,288,500.00 badala ya Shs. 25,830,000.00 na hivyo kuwapunja walimu kwa Shs 8,541,500.00.

Uchunguzi ulianzishwa kwa lengo la kubaini matumizi ya fedha hiyo ambayo haikulipwa na kama malipo yaliyofanywa kwa walimu yalizingatia Sheria na kanuni za kudumu za utumishi pamoja na waraka wa utumishi wa umma.
Imebainika kuwa malipo ya posho za kujikimu kwa walimu hao wa ajira mpya ambayo haikulipwa ilikusudiwa kutumiwa na Idara ya elimu ya halmashauri ya wilaya ya Mtama kwa matumizi tofauti na posho ya kujikimu ya siku saba (7) na nauli ya usafiri wa umma kwa kila

mtumishi aliyeajiriwa kwa kuzingatia mahali alipotoka. Baada ya TAKUKURU kuingilia kati fedha hiyo Shs 8,541,500.00 zimelipwa kwa walimu hao.

2. UZUIAJI RUSHWA

2.1 UFUATILIAJI WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

Katika kipindi tajwa, tumeendelea na ufuatiliaji wa utekelezwaji wa miradi **6** ya maendeleo yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni **118 (118,138,348,947.70)** katika sekta za Elimu, Maji na Kilimo. Miradi 3 ilikutwa na mapungufu madogo madogo ambayo hatua mbalimbali zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na kurekebisha mapungufu hayo.

2.2 WARSHA ZA WADAU

Warsha **6** za kujadili matokeo ya uchambuzi wa mifumo kwa kushirikisha wadau zilifanyika katika sekta za Ardhi, TASAF/Utawala na Maliasili ambapo maazimio ya namna ya kuziba mianya ya rushwa yalifikiwa na muda wa utekelezaji kuwekwa. Taarifa ya mfumo uliofanyiwa uchambuzi na yaliyobainika upo katika **kiambatisho Na. 1**

3. UELIMISHAJI UMMA

Mkoa wa Lindi umeendelea kutekeleza jukumu hilo kikamilifu kwa kuwahamasisha wananchi wote kushirikiana na TAKUKURU katika kuzuia vitendo vya rushwa hasa tunapoelekea katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa Novemba 2024.

Kazi za uelimishaji umma zilizofanyika ni kutembelea na kuimarisha klabu za wapinga rushwa 76 na kufungua klabu mpya 3 katika Shule za Msingi, Sekondari na Chuo, mikutano ya hadhara 67, semina 49, vipindi vya redio 11, uandishi wa makala 13, Mjadala wa wazi 1 na maonesho 6.

4. UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA TAKUKURU RAFIKI

Katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2024 program ya TAKUKURU Rafiki iliendelea kutelezwa Mkoani Lindi, na tulipokea kero zilizohusu sekta ya ujenzi, Elimu, TASAF, Afya, Ardhi, Nishati na Maji ambapo tulizitafutia ufumbuzi na kisha tukatoa mrejesho kwa wanufaika wa huduma kama zinavyoainishwa katika **Kiambatanisho Na. 2.**

5. UCHUNGUZI

Taarifa za malalamiko yaliyopokelewa katika kipindi hiki ni 61, ambapo malalamiko yasiyohusu rushwa ni 09 na yanayohusu rushwa 52 kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na 3.**

Malalamiko yasiyohusu rushwa walalamikaji walishauriwa na malalamiko hayo kufungwa na kwa yale ambayo yalihusu rushwa uchunguzi unaendelea na uko katika hatua mbalimbali.

6. MASHITAKA

Katika kipindi hicho shauri jipya **1** lilifunguliwa na kufanya jumla ya mashauri **(3)** yanayoendelea mahakamani kwa sasa.

7. UDHIBITI WA RUSHWA KUELEKEA UCHAGUZI

Katika kipindi hiki cha kuelekea uchaguzi wa Serikali za Mitaa Novemba 2024 na Uchaguzi Mkuu 2025 TAKUKURU Lindi imeendelea kudhibiti vitendo vya rushwa kwa kuwaelimisha wananchi kuhusu kutambua thamani ya kura yake, athari za rushwa katika uchaguzi pamoja na kuzingatia misingi ya haki, usawa, uwazi, uwajibikaji na uzalendo ili kuzuia upatikanaji wa viongozi wasio waadilifu wanaojihusisha na vitendo vya rushwa.

8. MIKAKATI YA 2024 - 2025

Tumepanga kuendelea kutekeleza majukumu yetu ya kudhibiti vitendo vya rushwa kwa mwaka wa fedha 2024/2425 kwa kufanya ufuatiliaji utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa ndani ya mkoa wa Lindi. Ufuatiliaji utasaidia kubaini kama miradi iliyotekelezwa inaendana na thamani ya fedha iliyotumwa.

Pia tumejipanga, kufanya warsha na wadau, kujadili matokeo ya chambuzi za mifumo zilizokamilika na kuweka maazimio ya namna bora ya kuziba mianya ya rushwa itakaobainishwa, ufuatiliaji wa karibu wa ukusanyaji wa mapato katika halmashauri pamoja na ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika maeneo ya ushirikiano wa mapambano dhidi ya rushwa. Sambamba na hayo, tutachukua hatua stahiki kwa wale watakaobainika kufuja mali za umma.

Aidha, tunatarajia kuongeza juhudi ya kuzuia rushwa kwa kuhamasisha ushiriki wa wananachi kupitia nyenzo mbalimbali za uelimishaji umma katika kudhibiti vitendo vya rushwa kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 2024 na Uchaguzi Mkuu wa 2025. Wananchi watahamasishwa kutambua thamani ya kura yao ili wasirubuniwe kwa hongo au vishawishi vyovyote vile na kudhalalisha utu wao kwa kupokea rushwa ili wamchague kiongozi asiyefaa au wasigombee/ kujitoa au kupiga kura.

Pia kupitia programu ya **TAKUKURU Rafiki** tutaendelea kuwashirikisha wananchi ambao ni wanufaika wa huduma kutambua kero na kuzipatia ufumbuzi katika maeneo ya kata zao. Kero hizi ni zile ambazo zikiachwa bila kupatiwa ufumbuzi zinaweza kusababisha kutokea kwa vitendo vya rushwa.

9. WITO KWA WAKAZI WA MKOA WA LINDI

Tunawashukuru wananchi, Vyombo vya Habari pamoja na Taasisi mbalimbali (za Serikali na binafsi) katika Mkoa wa Lindi kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kutupatia.

Ninawaomba wadau wetu wote muendelee kutuunga mkono kuzuia vitendo vya rushwa visitokee hasa tunapoelekea katika uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 na Uchaguzi Mkuu wa 2025, kwa kutoa taarifa wanapoona kuna viashiria vya rushwa ili tufanyie kazi kwani; TAKUKURU TUNASEMA: **"Kuzuia Rushwa ni Jukumu Lako na Langu, Tutimize Wajibu Wetu"**

Imetolewa na:

A. A. Kwariko,
Kaimu Mkuu wa TAKUKURU (M) LINDI
0738150118

Kiambatanisho Na 1.

UCHAMBUZI WA MFUMO

S/N	SEKTA	YALIYOBAINIKA	MAKUBALIANO YA UTEKELEZAJI
1	Ardhi	Waombaji kutokufanya malipo kwa wakati na hivyo kupelekea zoezi la upimaji, kupewa hati miliki au utatuzi wa migogoro kuchelewa	Waombaji wameelimishwa umuhimu wa kufanya malipo kwa wakati ili wasicheleweshewe huduma.
		Utoaji wa vibali vya ujenzi usioridhisha halmashauri ya wilaya ya Liwale.	Mamlaka ya upangaji inaendelea kutoa elimu kwa wananchi sambamba na kuwaandikia barua watendaji wa vijiji na kata ili kuwakumbusha wananchi kuzingatia taratibu za ujenzi
2	TASAF	Wanufaika kutokufahamu kuhusu mpango wa TASAF unavyofanya kazi	Wanufaika wemeanza kuelimishwa mpango wa TASAF unavyotekelezwa kwa kaya masikini
		Baadhi ya wanufaika kushindwa kumudu kazi za jamii kutokana na uzee na ugonjwa	Marekebisho ya mara kwa mara ya kaya yameanza kufanyika ili kubaini watu waliokusudiwa kufaya kazi jamii katika kaya husika kama bado wapo.
3	Maliasili	Baadhi ya wavunaji kutumia leseni za watu wengine kuvuna mazao ya misitu.	Kwa sasa uhakiki unafanyika ili mvunaji avune kwa kutumia leseni yenye jina lake,
		Baadhi ya magogo yaliyovunwa kusafirishwa kutoka eneo yalipovunwa bila kuwa na kibali cha kusafirishia.	Usimamizi wa sheria za uvunaji na usafirishaji magogo unazingatiwa kwa sasa.
		Baadhi ya leseni za uvunaji kutolipiwa kama utaratibu wa kisheria unavyoelekeza.	Uhakiki unafanyika kupitia bank statement kujiridhisha malipo kufanyika kabla ya leseni kutolewa.
		Leseni kulipiwa kwa majina tofauti na yale yanasomeka kwenye leseni husika	Malipo yote kwa sasa yanafanyika kwa jina la mwenye leseni

KIAMBATISHO Na. 2.

UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA TAKUKURU RAFIKI

Na.	KERO ZILIZOIBULIWA	SEKTA	UTATUZI ULIOKAMILIKA
1	Hakuna vivuko vya watembea kwa miguu barabara za mitaani kata ya Majengo Mtama.	Ujenzi	Vivuko vya watembea kwa miguu vimewekwa katika barabara hizo
2	Hawajalipwa fidia ya maeneo yao yaliyomegwa kwa ajili ya kupisha ujenzi wa barabara za mitaani kata ya Majengo Mtama		Barabara za mitaani hazina fidia kwa wanaoachia maeneo yao. Wananchi wamekubali kuwa utaratibu wa kushirikishwa na TARURA ulifanyika na wao wakaridhia.
3	Barabara za mitaani hazichongwi na hazieleweki.		Barabara saba zenye kilometa tano zimefanyiwa kazi na zitajengwa kwa kiwango cha lami mwaka 2024/25.
3	Kutokamilika kwa jengo la uthibiti ubora elimu Mtama.	Elimu	Ukamilisha wa jengo unaendelea baada ya kupatikana fedha iliyoombwa na liko katika hatua ya umaliziaji.
4	Wanufaika wa TASAF wameondolewa kwenye Mpango.	TASAF	Wamekidhi vigezo vya kuondolewa kwenye mpango wa kaya masikini.

5	Kuchelewa kwa malipo ya TASAF		Ulipwaji wa fedha kwa wanufaika ufuata madirisha ya ulipaji, na tarehe za malipo upangwa na TASAF makao makuu. Fedha inapopokelewa halmashauri ulipwa kwa wakati.
6	Hakuna dawa kituo cha afya cha mji Manispaa ya Lindi.	Afya	Kwa sasa hakuna tatizo hilo baada ya kufanyiwa kazi kwa kupunguza muda wa kuagizwa dawa toka miezi 6 hadi miezi 2.
7	Ucheleweshaji wa upatikanaji wa hati miliki Manispaa ya Lindi.	Ardhi	Hakuna ucheleweshaji kwa hati mpya isipokuwa kwa nyumba za urithi ambazo zinahitaji kujiridhisha kwa kuwa mara nyingi ndugu hawashirikishani wakati wa kuuza.
8	Kuchelewesha kuunganisha umeme	Nishati	Tatizo hilo halipo kwa sasa baada ya kupunguza kuonana na malipo kufanywa kupitia mfumo.
9	Mapato na matumizi ya maji hayasomwi kata ya Namangale	Maji	CBWSO zimesisitizwa kuandaa taarifa na kusomwa kwa wananchi kwa kila robo ya mwaka na utekelezaji umeanza
10	Wajumbe wa kamati za MAJI (CBWSO) hawalipi maji na wanauza maji kwenye nyumba zao – Namangale.		Viongozi waliobainika kutumia maji bure wameamriwa kulipa faini na kuondolewa katika nyadhifa zao.

Kiambatisho Na 3.
UCHUNGUZI MKOA WA LINDI(APRILI-JUNI)

Na	SEKTA ZINAZOHUSIKA	MALAMIKO YALIYOHUSU RUSHWA	MALALAMIKO YASIYOHUSU RUSHWA
1	TAMISEMI	18	1
2	ELIMU	6	
3	USHIRIKA	9	2
4	POLISI	0	1
5	AFYA	4	
6	MAENDELEO JAMII	3	1
7	MAJI	1	
8	USAFIRISHAJI NA UCHUKUZI	2	
9	ARDHI	3	2
10	UVUVI, KILIMO NA MIFUGO	4	
11	MISITU		1
12	BIASHARA	0	1
13	MAHAKAMA & MASHTAKA	2	
	JUMLA	**52**	**09**